

Bibilia ya watoto  
Inawalettea

Miujiza ya Yesu



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Byron Unger; Lazarus  
Alastair Paterson

Imerekebishwa na: E. Frischbutter; Sarah S.

Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,  
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya

Kimedhibitishwa na: Bible for Children  
[www.M1914.org](http://www.M1914.org)

©2023 Bible for Children, Inc.


License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.



Yesu alifanya miujiza mingi. Miujiza ilikuwa ni ishara ya kuonyesha kuwa hakika Yesu ni Mwana wa Mungu. Muujiza wa kwanza ulitokea kwenye sikukuu ya harusi. Tatizo lilitokea. Hapakuwa na divai ya kutosha kwa ajili ya kila mtu.



Mariamu, mama yake Yesu, alimwambia kuhusu tatizo hilo, kisha akawaambia watumishi wafanye lolote watakalomagizwa na Yesu.



Yesu alisema "Jalizeni haya mabalasi maji." Pengine waliuliza, "Maji?" Ndiyo, alichohitaji Yesu ni maji.



Kisha Yesu alimwambia  
mtumishi ateke maji  
kwenye balasi moja  
kubwa na kumpelekea  
mkuu wa meza aonje.  
Sasa maji yalikuwa  
yamebadilika kuwa  
divai! Divai  
njema! Divai  
bora!



Watumishi walishangaa.  
Yesu alikuwa ameyabadili  
maji kuwa divai. Ni  
Mungu tu anayeweza  
kufanya miujiza  
kama hiyo.




Yesu alifanya miujiza mingine.  
Jioni moja, Yeye na wanafunzi  
Wake walienda nyumbani kwa  
Petro. Mkwe wa Petro alikuwa  
ameshikwa na homa kali.





Yesu aligusa mkono wa huyu mwanamke mgonjwa.  
Mara akapona. Akainuka na kumtumikia Yesu na  
wanafunzi.



Inavyoonekana mji  
wote ulikusanyika  
mlangoni jioni hiyo.  
Wagonjwa walikuja  
- vipofu, viziwi,  
bubu, vilema. Hata  
watu wenye mapepo  
walimkusanyikia  
Yesu. Aliweza  
kuwasaidia  
watu wengi  
kiasi hicho?



Yesu, Mwana wa Mungu, aliweza kusaidia. Yesu alisaidia. Wote waliomwendea waliponywa. Watu ambao walikuwa wanajiburuta kwa magongo sasa waliweza kutembea na kukimbia na kuruka.




Wengine walikuja,  
ambao waliharibiwa  
sura zao na ukoma.



Wakawa wazima na  
safi kwa vile Yesu  
aliwaponya.



Wanaume na wanawake waliosumbuliwa na mapepo walisimama mbele ya Yesu. Aliwaamuru mapepo watoke. Wakati mapepo wakitii, watu wenye hofu, wasio na furaha wakawa watulivu na wenye furaha.



Nyuma ya umati wa watu, watu wanne walijaribu kumsaidia rafiki yao afike kwa Yesu. Lakini hawakuweza kufika karibu. Wangeweza kufanya nini?



Marafiki wanne wenye imani  
walimpandisha mgonjwa kwenye  
paa la nyumba, wakalipasua  
paa na kumshusha  
chini. Sasa alikuwa  
karibu na Yesu.





Yesu aliona kwamba wale marafiki wanne walikuwa na imani. Akamwambia mgonjwa, "Umesamehewa dhambi zako. Jitwike godoro lako uende." Mtu huyo alisimama, vizuri akiwa imara. Yesu alikuwa amemponya.



Muda mfupi baadaye, Yesu alikuwa katika mashua pamoja na wanafunzi. Dhoruba ya kutisha iliipiga bahari. Yesu alikuwa amelala. Wanafunzi wenye hofu walimuamsha. Walilia, "Bwana, tuokoe." "Tunaangamia!"



Yesu aliukemea upepo, "Nyamaza, utulie." Mara moja, bahari ikatulia. Wanafunzi wake wakamaka, "Huyu ni mtu wa namna gani?" Hata upepo na bahari vinamtii. Waliamini Yesu alikuwa Mwana wa Mungu kwa sababu miujiza yake ilionyesha utukufu Wake. Wanafunzi hawakujua,

lakini walikuwa wakitarajiwa kumwona Yesu akifanya miujiza mikubwa zaidi akimtumikia Mungu kati ya wanadamu.



# Miujiza ya Yesu

Hadithi kutoka katika Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Mathayo 8-9, Marko 1-2, Marko 4,  
Luka 4, Luka 8, Yohana 2

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."  
Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma Mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atakuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Tamka maneno haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

